**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**634** **STADI ZA KAZI**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A**, **B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila Sehemu **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Eleza kwa kifupi maana ya kimia.
   (b) Taja vifaa sita (6) vinavyotumika katika kuchapa kwa njia ya kimia.

2. Taja kanuni nne za upigaji wa picha tuli zinazotakiwa kupitiwa na mwalimu kabla ya kuanza kufundisha mada hiyo darasani.

3. Onesha kwa hoja nne faida za muziki katika jamii.

4. Eleza kwa kifupi aina nne za majadiliano zinazoweza kutumika kufundisha mada ya Ususi.

5. Ainisha hatua nne za kufuata katika kuhakikisha usafi na usalama wa chakula jikoni.

6. Orodhesha vifaa nane vitakavyowasaidia kuwawezesha wanafunzi wao kupata stadi ya utarizi.

7. Kubainisha njia nne za kudumisha afya njema ya wanyama wanaofugwa.

8. Onesha udhaifu wa mbinu ya kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya udobi, kwa hoja nne.

9. (a) Eleza kwa kifupi njia mbili za utunzaji wa picha.
   (b) Kwa kutoa hoja mbili, eleza sababu za kutunza picha.

10. Tofautisha kati ya ujuzi na lengo mahsusi kama vinavyotumika katika Andalio la Somo.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

11. (a) Fafanua sababu mbili za kufanya matengenezo ya viatu.
    (b) Eleza hatua nne za kufuata katika kukadiria gharama ya vifaa vya kufanyia matengenezo ya viatu.

12. Chambua hatua sita za kufuata katika kushona kifani cha kofia.

13. Fafanua aina sita za mitindo ya ushonaji wa sketi.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

14. (a) Eleza umuhimu wa msingi wa weledi wa matumizi na uhifadhi wa mazingira na jamii katika ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi, kwa kutoa hoja mbili.
    (b) Fafanua matumizi matatu ya msingi wa weledi wa matumizi na uhifadhi wa mazingira na jamii katika ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi.

15. Eleza mambo sita muhimu ya kuzingatia katika kuandaa zana za upimaji wa somo la Stadi za Kazi.

16. Chambua hatua sita za kufuata wakati wa kufundisha Uigizaji kwa wanafunzi wa Darasa la Sita.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org